




WIZARA YA AFYA
TAASISI YA CHAKULA NA LISHE TANZANIA



TAARIFA KWA UMMA

**UFAFANUZI KUHUSU ASILIMIA 43 YA CHUMVI INAYOZALISHWA NCHINI
KUKOSA MADINI JOTO**

Katika Gazeti la Nipashe la Ijumaa Tarehe 25 Februari, 2022 Na.0580867 katika ukurasa wa mbele (Front Page) ilitoa taarifa yenye kichwa kinachosema **ASILIMIA 43 YA CHUMVI NCHINI NI HATARI**, taarifa hii imeleta taharuki kwa Viongozi, wadau na wananchi kwa ujumla na kuleta maswali mengi kwa Taasisi ya Chakula na Lishe Tanzania kutaka kujuu kwamba ni hatari gani iliyopo kwenye chumvi inayozalishwa nchini.

Mwaka 2019 Taasisi ya Chakula na Lishe Tanzania kwa kushirikiana na wadau ilifanya utafiti wa Sekta ya chumvi uliobaini kuwa Tanzania inazalisha chumvi tani 330,712 kwa mwaka. Kati ya chumvi hiyo, kiasi cha tani 141,228 ambapo ni sawa na asilimia 43 ya chumvi iliyoko sokoni hakiwekwi madini joto ya kutosha.

Aidha, utafiti huo ulibaini kwamba chumvi nyingi isiyo na madini joto inatoka kwa wazalishaji chumvi wadogo. Tanzania inakadiriwa kuwa na wazalishaji wadogo wa Chumvi zaidi ya 7000 wanaotumia teknolojia duni za kuzalisha chumvi na wametawanyika katika maeneo mbalimbali ambayo hayafikiki kwa urahisi.

Kutokana na changamoto hiyo, Wizara ya Afya kupitia Taasisi ya Chakula na Lishe Tanzania kwa kushirikiana na wadau wetu ilianzisha Mpango Jumuishi wa uchanganyaji wa madini joto kwenye chumvi kwa kutumia mashine za kisasa za ambazo zinatolewa kwa mikoa inayozalisha chumvi kwa wingi nchini.

Zoezi hili lilianza mwaka 2018, ambapo jumla ya mashine tatu zenyet thamani ya jumla ya shilingi 75,000,000/- zilitolewa na kusimikwa katika halmashauri tatu za Kilwa, Meatu na Hanang. Mwaka huu (2022) jumla ya mashine tano zenyet thamani ya shilingi milioni 55 zimetengenezwa hapa hapa nchini na wataalamu kutoka VETA ambapo makabidhiano kwa mikoa mitatu ya Tanga, Pwani na Mtwara yalifanyika Mkoani Dodoma.

Lengo la kugawa mashine hizo ni kuwawezesha wazalishaji wadogo wa chumvi kuongeza madini joto ya kutosha kwenye chumvi wanayozalisha ili kufikia angalau asilimia tisini (90%) ya kaya zote nchini zinatumia chumvi yenye madini joto ya kutosha kama inavyopendekezwa na shirika la afya duniani (WHO).

Taasisi inatoa wito kwa wananchi wote kuendelea kutumia chumvi iliyochanganywa na madini joto ambayo inapatikana maeneo yote nchini kwa kuangalia kifungashio chenye nembo maalumu inayoonesha kuwa chumvi hiyo imeongezwa madini joto. Nembo yenye ni kama inavyoonekana hapo chini.



Imetolewa na:

Jackson E. Monela
Afisa Uhusiano wa Umma